

**LASJET EXAMINATIONS**

JINA \_\_\_\_\_ Nambari: \_\_\_\_\_  
Sahihi: \_\_\_\_\_  
Tarehe: \_\_\_\_\_

**102/3**

**KISWAHILI**

**FASIHI YA KISWAHILI**

**2020 FORM 4 TERM 1 END TERM EXAMS**

**MUDA: SAA  $2\frac{1}{2}$**

**MAAGIZO:**

- 1.Jibu maswali MANNE Pekee.
- 2.Swali la kwanza ni la lazima.
- 3.Maswali mengine yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki.
- 4.Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
- 5.Kila swali lina alama ishirini

### **1. SEHEMU A: USHAIRI (LAZIMA)**

Eti

Mimi niondoke hapa  
Niondoke hapa kwangu  
Nimesaki, licha ya risasi  
Vitisho na mauaji, siondoki

Mimi

Siondoki  
Siondoki siondoki  
Niondoke hapa kwangu!  
Kwa mateke hata na mikuki  
Marungu na bunduki, siondoki

Hapa

Siondoki  
Mimi ni Pahame!  
Niondoke hapa kwangu!  
Fujo na ghasia zikizuka  
Na kani ya vaporaji, siondoki

Haki

Siondoki  
Kwangu siondoki  
Niondoke hapa kwangu!  
Nawaje; waje wanaokuja  
Mabepari wadhalimu, siondoki

Kamwe

Siondoki  
Ng'oo hapa kwangu!  
Katizame chini mti ule!  
Walizikwa babu zangu, siondoki

Sendi

Nende wapi?  
Si hapa kitovu changu  
Niondoke hapa kwangu  
Wangawa na vijikaratasi  
Si kwamba hapa si kwangu, siondoki

Katu

Siondoki

Sihitaji karatasi  
Niondoke hapa kwangu  
Yangu mimi ni ardhi hii  
Wala si makaratasi, siondoki

### **Maswali**

- a) Shairi hili ni la aina gani? Kwa nini (alama 2)
- b) Taja masaibu anayopitia mzungumzaji (alama 4)
- c) Eleza toni ya shairi hili (alama 2)
- d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 3)
- e) Tambua matumizi ya mbinu ya usambamba (alama 2)
- f) Andika ubeti wa tano kwa lugha nathari (alama 4)
- g) Tambua idhini moja ya mtunzi (alama 1)
- h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivytumika katika shairi (alama 3)
  - (i) Karatasi (al. 4)
  - (ii) Nimesaki (al. 2)
  - (iii) kitovu (al. 1)

### **2SEHEMU B TAMTHILIA YA KIGOGO**

2.Uliona nini kwa huyo zebe wako ? Eti mapenzi!

- a. Eleza muktadha wa dondo. (al. 4)
- b. Andika mbinu za lugha zinazojitokeza kwenye dondo hili (al. 4)
- c. Taja hulka za mnenaji unajitokeza katika dondo. (al. 2)
- d. Mwanamke ni kiumbe wa kukandamizwa. Thibitisha kauli hii ukirekjelea tamthilia. (al. 10)

3.wa kurejelea tamthilia ya 'Kigogo ya Pauline Kea, onyesha jinsi ambavyo viongozi wengi katika nchi za Kiafrika wamejawa na tamaa. (alama 20)

### **SEHEMUC.RIWAYA YA CHOZI LA HERI(ASSUMPTA MATEI)**

4.“ Kwa kweli ni hali ngumu hii”

Weka dondo katika muktadha wake. (alama4)

Ni hali gani yamsemewa inayorejelewa kwenye dondo. (alama16)

5) Ukabila ni tatizo sugu katika nchi nyingi za Kiafrika. Tetea kauli hii ukilejelea Chozi la Heri ( al. 20)

**Alifa Chokocho na Dumu Kayanda: Tumbo Lisiloshiba na Hadithi nyingine**

**jibu swalı la 6 au la 7**

6.Ukirejelea hadithi zifuatazo, eleza jinsi maudhui ya mapenzi na asasi ya ndoa yanavyojitokeza.  
(alama20)

- a) Mapenzi ya kifaurongo
- b) Masharti ya kisasa
- c) Ndoto ya Mashaka
- d) Mtihani wa maisha

Au

**Shibe inatumaliza : Salma Omar Hamad**

7.“Hiyo ni dharau ndugu yangu. Kwa nini kila siku tunakula sisi kwa niaba ya wengine ?”

- a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
- b)Eleza sifa za msemaji. (alama 6)
- c) Eleza jinsi viongozi wanavyokuwa wabahirifu. (alama 10)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

- 8a) Fafanua mchakato/formula ya uwasilishaji wa vitendawili. (alama4)
- b) Linganisha naulingenue vitendawili na methali. (alama10)
- c) Toa sababu sita za kudidimia kwa fasihi simulizi. (alama6)